

# ثلاثة الأصول

## MISINGI MITATU

MTUNZI:

SHEIKH MUHAMMAD IBN  
SULEIMAN AT-TAMIMY

MFASIRI:

ABU HALIMA ARAFAT IBN MAHMOUD

## **UTANGULIZI WA MHAKIKI**

Sifa njema zote zinamstahiki Allaah mtukufu, na Swala na Salamu Zimfikie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake pamoja na Maswahaba zake.

Baada ya utangulizi huo: katika yaliyo wajibu kwa kila muislamu mwanamme na mwanamke, awe mdogo au mkubwa ni kutilia umuhimu swala zima la Aqida (Itikadi) na kulipa kipaumbele hasa katika zama zetu hizi, kwani itikadi nyingi potofu zimedhihiri ambazo zinapoteza watu na kuwatoa katika itikadi sahihi aliyokuja nayo Mtume wetu Swala na Salamu Zimfikie.

Na kitabu hiki kilichotungwa na sheikh wa Uislamu Muhammad At Tamimiy Allaah amrehemu ni katika vitabu ambavyo maulamaa wamehimiza kwamba waislamu waanze kujifunza Aqida yao sahihi kwa kitabu hiki (**Al-Usuulu Tthalaatha**) ambacho mtunzi wake ameweka wazi nguzo za Aqida ya Uislamu na kutaja dalili zenye nguvu kutoka katika Qur'an na Hadithi sahihi.

Kitabu hiki kimetafsiriwa kwa lugha nyingi, lakini tafsiri hii ya lugha yetu ya Kiswahili aliyoiandika ndugu yetu Abu Halima Arafat Allaah amuhifadhi ni tafsiri nzuri na nyepesi kufahamu kwa kila anaejuwa lugha ya Kiswahili.

Allaah amlipe ndugu yetu huyu kila la kheri na amzidishie ilimu kwa juhudi hii aliyotoa ya kutafsiri kitabu hiki.

Swala na Salamu Zimfikie Mtume wetu Muhammad,  
Jamaa zake pamoja na Maswahaba zake.

**Ameandika:**

**Abu Hashim Abdul Qadir**  
**9/Jumaadal Uulaa/1439H – 26/1/2018M.**  
**Mombasa Kenya**

## بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ

Juwa Allaah akurehemu, ni wajibu kujifunza mambo manne:

**Jambo la kwanza:** kujifunza elimu, nayo ni kumjua Allaah, Mtume wake Swala na Salamu Zimuendee, na kuijua dini ya kiislamu kwa hoja na dalili.

**Jambo la pili:** kuifanyia kazi (ilimu hiyo).

**Jambo la tatu:** kulingania kwenye elimu hiyo (kuifundisha).

**Jambo la nne:** kusubiri juu ya yale yatakayokusibu.

Na dalili (juu ya mambo hayo manne) ni kauli yake Allaah:

﴿ وَالْعَصْرِ ﴿ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ ﴿ إِلَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَّصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَّصَوْا بِالصَّبْرِ ﴾

[Naapa kwa zama\* Hakika binaadamu (bila ya shaka) yumo katika khasara,\* ila wale walioamini na wakatenda mema, wakausiana kwa haki na wakausiana kusubiri!].

---

<sup>1</sup>- Surat Al Asr/ 1-3

Amesema imamu Shafii' (Allaah amrehemu): “Lau Allaah asingewateremshia waja wake hoja yoyote isipokuwa sura hii tu, basi ingewatosheleza<sup>2</sup>).

Na amesema imamu Bukhari Allaah amrehemu katika sahihi yake:

(بَابُ: الْعِلْمُ قَبْلَ الْقَوْلِ وَالْعَمَلِ)

(Huu ni mlango: Elimu kabla ya kauli na amali).

Na dalili (kuwa ni wajibu kutanguliza elimu) ni kauli ya Allaah:

﴿فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ﴾

(Basi jua ya kwamba hapana Mola ila Allaah, na Omba Msamaha kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake<sup>3</sup>).

(Allaah) ameanza kwa amri ya kusoma kabla ya kusema wala kutenda amali yoyote.

---

<sup>2</sup>- Makusudio yake ni: Lau Allaah asingewateremshia waja wake hoja yoyote (katika Qur'an) yenye kubainisha sababu za kufaulu, kupata utukufu, kuepukana za kuangamia na kupata hasara, isipokuwa surat Al-Asr basi ingewatosheleza katika kubainisha hilo, na Qur'an yote ni yenye kuyaelezea mambo haya manne kwa mchanganuo, kama alivyoitaja faida hiyo Sheikh Fauzaan Allaah amhifadhi katika sharhi ya kitabu hiki: (Uk: 36-37).

- Amesema Imamu An-Nawawiy Allaah amrehemu: Amesema Imamu Shafii Allaah amrehemu: “Watu wameghafilika na sura hii”. Al-Majmuu: (Jz. 1, Uk. 29).
- Amesema ibnul Qayyim: “Amesema imamu Shafii: lau watu wote wangeitafakari sura hii ingewatosha; kwa sababu ukamilifu wa mtu upo kwenye ukamilifu wa nguvu yake kielimu na matendo ambayo ni imani nzuri, na kama ilivyo wajibu mtu kuitafutia nafsi yake ukamilifu basi ni wajibu vile vile kuitafutia nafsi ya mwingine ukamilifu, na huko ndio kuusiana kwa haki na kuusiana (kuwa na) subra, na misingi ya muhimili wake ambao juu yake litasimama jambo hili si subra”. Madaariju Ssaalikin: (Jz. 1, Uk. 6).

<sup>3</sup>- Surat Muhammad /19.

Juwa Allaah akurehemu, ya kwamba ni wajibu juu ya kila Muislamu mwanaume na mwanamke, kujifundisha mambo haya matatu na kuyafanyia kazi:

**Jambo la kwanza:** Allaah ndiye aliyetuumba na kuturuzuku, wala hakutuacha bure bure, bali ametuletea sisi Mtume Muhammad Swala na Salamu Zimfikie, mwenye kumtii ataingia peponi na mwenye kumuasi ataingia motoni.

Na dalili ni kauli ya Allaah:

﴿ إِنَّا أَرْسَلْنَا إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَا أَرْسَلْنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ رَسُولًا \* فَعَصَىٰ فِرْعَوْنُ الرَّسُولَ فَأَخَذْنَاهُ أَخْذًا وَبِيًّا ﴾

(Hakika sisi tumemtuma kwenu Mtume hali ya kuwa ni shahidi juu yenu, kama tulivyo mtuma Mtume kwa Firauni\* Lakini Firauni alimuasi huyo Mtume, basi tukamshika mshiko wa mateso<sup>4</sup>).

**Jambo la pili:** Allaah haridhii kushirikishwa pamoja nae (kiumbe) yoyote katika ibada zake, si Malaika waliokurubishwa (kwa Allaah), wala Nabii yeyote aliyetumwa.

Na dalili ni kauli ya Allaah:

﴿ وَأَنَّ الْمَسْجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا ﴾

(Hakika misikiti ni ya Allaah, basi msimuabudu yoyote pamoja na Allaah<sup>5</sup>).

---

<sup>4</sup>- Surat Muzzammil/15-16.

<sup>5</sup>- Suratul Jinn/18/

**Jambo la tatu:** yeyote mwenye kumtii Mtume Swala na Salamu Zimfikie, na akampwekesha Allaah basi haifai kwake kumfanya kipenzi yule mwenye kumpiga vita Allaah na Mtume wake Swala na Salamu Zimfikie, ijapokuwa ni jamaa wa karibu.

Na dalili ni kauli yake Allaah:

﴿ لَا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ، وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ  
أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أُولَئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ مِّنْهُ  
وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ  
أُولَئِكَ حِزْبُ اللَّهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴾

(Huwakuti watu wanaomuamini Allaah na siku ya mwisho kuwa wanawapenda wanao mpinga Allaah na Mtume, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao ameandika katika nyoyo zao Imani, na amewapa nguvu kwa roho itokayo kwakwe. Na atawaingiza katika mabustani ipitayo chini yake mito. Hali ya kukaa humo milele. Allaah awe radhi nao na wao wawe radhi nae. Hao ndio Hizbullaah 'kundi la Allaah', hakika kundi la Allaah ndilo lenye lenye kufaulu<sup>6</sup>).

\*\*\*\*\*

---

<sup>6</sup>- Surat Al-Mujaadalah /22.

## Nini maana ya Haniifiyya?<sup>7</sup>

Jua Allaah akuongoze katika twaa' yake, hakika Haniifiyya (ambayo ni Mila ya Nabii Ibrahim) Swala na Salamu Zimfikie, ni: Kumuabudu Allaah pekee na kumtakasia yeye dini, na Allaah amewaamrisha watu kufanya jambo hilo, na akawaumba kwa ajili hiyo kama Allaah alivyosema:

﴿وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ﴾

(Na sikuwaumba majini na watu isipokuwa waniabudu Mimi<sup>8</sup>).

Na maana ya neno (يَعْبُدُونَ) ni: Wampwekeshe.

Na jambo kubwa kabisa ambalo Allaah ameliamrisha ni Tawhiid, nayo ni: kumpwekesha Allaah katika ibada.

Na jambo kubwa kabisa ambalo Allaah amelikataza ni shirki, nayo ni: kumuabudu pamoja naye mwengine (katika viumbe wake). Na dalili ni kauli yake Allaah:

﴿وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا﴾

(Muabuduni Allaah, wala msishirikishe na chochote<sup>9</sup>).

**Ukiulizwa:** Ni ipi misngi mitatu ambayo ni lazima kwa mwanadamu kuijua?

**Sema:** Ni mja kumjua Mola wake mlezi, na dini yake, na kumjua Mtume wake Muhammad Swala na Salamu Zimfikie.

---

<sup>7</sup>- Mtunzi wa kitabu hiki ameweka utangulizi wa aina tatu:

1. Juwa ni wajibu kujifunza mambo manne.
2. Juwa ni wajibu juu ya kila Muislamu mwanamme na mwammke, kujifundisha mambo matatu na kuyafanyia kazi.
3. Juwa maana ya Haniifiyya ni kumuabudu Allaah pekee na kumtakasia yeye Dini.

<sup>8</sup>- Surat Ad-Dhaariyaat/56.

<sup>9</sup>- Surat An-Nisaa/36.

## **Msingi wa kwanza Mja kumjua Mola wake Mlezi**

**Ukiulizwa:** Ni nani Mola wako mlezi?

**Sema:** Mola wangu mlezi ni yule aliyenilea mimi, na kuwalea viumbe wote kwa neema zake, naye ndiye muabudiwa wangu, sina mimi muabudiwa mwingine ila yeye, na dalili ni kauli ya Allaah:

﴿الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾

**(Sifa njema zote ni za Allah, Mola mlezi wa viumbe vyote<sup>10</sup>).**

Na kila kisicho kuwa Allaah kimeumbwa, na mimi ni miongoni mwa hao viumbe.

**Ukiulizwa:** kwa kitu gani umemjua Mola wako?

**Sema:** tumemjua kwa ishara zake na viumbe wake.

Na miongoni mwa ishara zake ni: usiku, mchana, jua, na mwezi, na miongoni mwa viumbe vyake ni: mbingu saba, na ardhi saba, na vilivyomo ndani yake, na vilivyo baina yake; na dalili ni kauli ya Allaah Mtukufu:

﴿وَمِنْ آيَاتِهِ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ

الَّذِي خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ﴾

**[Na katika alama zake ni usiku na mchana, jua na mwezi. Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Allaah aliye viumba (hivyo), mkiwa nyinyi mnamuabudu yeye tu<sup>11</sup>].**

---

<sup>10</sup>- Surat Faatiha/2.

<sup>11</sup>- Surat Fuswilat/37.

Na kauli yake Allaah:

﴿ إِنَّ رَبَّكُمْ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشَىٰ  
الَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ  
وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ ﴾

(Hakika Mola wenu Mlezi ni Allaah aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha akalingana sawa juu ya Arshi. Huufunika mchana kwa usiku, unaoufuata haraka haraka<sup>12</sup>. Na jua, mwezi na nyota zinazo tumika kwa amri yake. Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Allaah, Mola Mlezi wa viumbe vyote<sup>13</sup>).

Na neno Rabbi maana yake ni: Muabudiwa, na dalili ni kauli ni:

﴿ يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ \*\* الَّذِي جَعَلَ  
لَكُمْ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَكُمْ  
فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَنْدَادًا وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴾

(Enyi watu, Muabuduni Mola wenu Mlezi ambaye amekuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka\*\* Mola ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa ni tandiko, na mbingu kama paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni, na akatoa kwayo matunda yawe riziki kwenu. Basi msimfanyie Allaah washirika, na hali nyinyi mnajua<sup>14</sup>).

<sup>12</sup>- Kila kimoja ni chenye kumfuata mwenzie (Vinapokezana) kwa haraka sana, ukitoka usiku unaingia mchana, na kama hivyo.

<sup>13</sup>- Surat A'raaf/54.

<sup>14</sup>- Surat Al-Baqara/

Amesema Ibn Kathir Allaah amrehemu: **“Aliye viumba vitu hivi ndiye anayestahiki kuabudiwa<sup>15</sup>”**.

Na aina za ibada ambazo Allaah ameamrisha, mfano: Uislamu, Imani, Ihsani, na miongoni mwa hizo ni: Dua, Hofu, Kutarajia, Kutegemea, Raghba (kuwa na pupa ya kufikia unalolipenda), Rahba (kuogopa ambako kuna mafungamano na elimu), Unyenyekevu, Woga, Kutubia, Kutaka msaada, Kuomba kinga, Kutaka kuokolewa, Kuchinja, Kuweka nadhiri, na nyingine miongoni mwa ibada ambazo Allaah ameziamrisha, ibada zote (hizo) afanyiwe Allaah pekee.

Na dalili (kwamba anayetakiwa kuombwa dua ni Allaah peke yake) ni kauli yake Allaah:

﴿وَأَنَّ الْمَسْجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللَّهِ أَحَدًا﴾

**(Na hakika misikiti ni ya Allaah, basi msimuabudu yeyote pamoja na Allaah<sup>16</sup>).**

Na yeyote atakaegeuza moja kati ya ibada hizo kwa kumfanyia asiyekuwa Allaah, basi huyo atakuwa ni mshirikina tena ni kafiri.

Na dalili nyingine ni kauli ya Allaah:

﴿وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ  
الْكَافِرُونَ﴾

---

<sup>15</sup>- Ametaja Ibn Kathir Allaah amrehemu katika tafsiri yake: **“Makusudio yake ni kwamba yeye ndiye Mwenye kuumba, kuruzuku, na ndiye Mmiliki wa ulimwengu, na vilivyomo, na ndiye anaewaruzuku, kwa hiyo anastahiki kuabudiwa bila kushirikishwa na chochote”**.

<sup>16</sup>- Surat Jinn/18.

(Na anaemuomba (pamoja na Allaah) Muabudiwa mwingine hana hoja wa hilo, basi bila ya shaka hisabu yake iko kwa Mola wake Mlezi. Kwa hakika hawatafaulu makafiri<sup>17</sup>).

Na imekuja katika hadithi:

«الدُّعَاءُ مُخِ الْعِبَادَةِ»

(Dua ni ubongo wa ibada<sup>18</sup>).

Na Allaah anasema:

﴿وَقَالَ رَبُّكُمْ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ﴾

(Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni. Kwa hakika wale ambao wanafanya kiburi kuniomba mimi wataingia Jahannamu wadhhalilike<sup>19</sup>).

Na dalili ya kwamba mtu anatakiwa kumhofu<sup>20</sup> Allaah peke ni:

﴿فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُوا اللَّهَ إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ﴾

---

<sup>17</sup>- Surat Muuminuun/117.

<sup>18</sup>- Miongoni mwa kasoro za hadithi hii:

1. Udhaifu wa Ibn Lahii'a'.
2. Walid Bin Muslim amehadithia kwa an-an hali ya kuwa anafanya tadliis. Na inatosheleza hadithi ya Nu'man Bin Bashir Allaah amridhie: **"Dua ni ibada"**. Tirmidh: (3372), Abu Daud: (1479) na ameisahihisha Sheikh Muqbil: (Al-Musnad: Jz. 2, Uk. 215

<sup>19</sup>- Surat Ghaafir/60.

<sup>20</sup>- Kuwa na hofu kumegawanyika:

1. Hofu ya kimaumbile, kama vile kuogopa moto n.k.
2. Hofu ya kumuogopa kiumbe mpaka ukafikia kumuabudu, ni sawa yuko hai au amaekufa, kama baadhi ya watu wanavyowafanyia wale wanaoitakidi kuwa ni Mawalii, Masharifu n.k, hii ni shirki.
3. Hofu ya kumuogopa Allaah kwa kuacha maasi, na aina hii ndio anayo ikusuduia mtunzi wa kitabu hiki.

(Basi msiwaogope, bali niogopeni mimi mkiwa nyinyi ni Waumini<sup>21</sup>).

Na dalili ya kwamba mtu anatakiwa atarajie kwa Allaah tu ni kauli yake:

﴿ فَمَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا ﴾

(Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi<sup>22</sup>).

Na dalili ya kwamba wa kumtegemea ni Allaah pekee ni:

﴿ وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴾

(Na kwa Allaah tu tegemeeni, mkiwa nyinyi ni Waumini<sup>23</sup>).

Na akasema:

﴿ وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ ﴾

(Na mwenye kumtegemea Allaah Yeye ni tosha yake<sup>24</sup>).

Na dalili ya kwamba Raghba, Rahba<sup>25</sup>, na Khushui (unyenyekevu) ni ibada, ni:

﴿ إِنَّهُمْ كَانُوا يُسْرِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا وَكَانُوا لَنَا خَشِعِينَ ﴾

(Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na wakituombakwa kwa shaukuna khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekoa<sup>26</sup>).

<sup>21</sup>- Surat Aal Imraan/175.

<sup>22</sup>- Surat Kahfi/110.

<sup>23</sup>- Surat Al-Maida/23.

<sup>24</sup>- Surat At-Ta'laaq/3.

<sup>25</sup>- **Raghba**: kuwa na pupa ya kulifikia jambo unalolipenda.

- **Rahba**: kuogopa kunakofungamana na kuwa na elimu juu ya kile unachokiogopa.

<sup>26</sup>- Surat Al-Anbiyaa/90.

Na dalili ya kwamba anaestahiki kuogopwa ni Allaah peke yake ni:

﴿فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي﴾

**(Basi msiwaogope wao, lakini niogopeni mimi<sup>27</sup>)**

Na dalili ya kwamba anaestahiki kurejewa kwa toba ni Allaah pekee ni:

﴿وَأَنِيبُوا إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلُمُوا لَهُ مِن قَبْلِ أَن يَأْتِيَكُمُ الْعَذَابُ ثُمَّ لَا تُنصَرُونَ﴾

**(Na rejeeni kwa Mola wenu Mlezi na jisalimisheni kwakwe<sup>28</sup>).**

Na dalili ya kwamba wakuombwa msaada ni Allaah pekee ni:

﴿إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ﴾

**(Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada<sup>29</sup>).**

Na imekuja hadithi inayosema:

«فَإِذَا اسْتَعْنَتْ فَاسْتَعْنِ بِاللَّهِ»

**(Unapotaka msaada muombe Allah<sup>30</sup>).**

Na dalili ya kwamba anaestahiki kutakiwa ulinzi ni Allaah peke yake ni:

﴿قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ﴾

**(Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa Mapambazuko<sup>31</sup>).**

---

<sup>27</sup>- Surat Al-Baqara/150.

<sup>28</sup>- Surat Az-Zumar/54.

<sup>29</sup>- Surat Al-Faatiha/5.

<sup>30</sup>- Tirmidh: (2516), na Ahmad; (2669), na wengine.

<sup>31</sup>- Surat Al-Falaq/1.

Na kauli yake:

﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴾

(Sema: Najikinga kwa Mola Mlezi wa wanaadamu<sup>32</sup>).

Na dalili ya kwamba Allaah pekee ndiye wa kuombwa msaada wa kuokolewa ni kauli yake Allaah:

﴿ إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَبَ لَكُمْ ﴾

(Kumbuka Mlipokuwa mkimuomba msaada mola wenu<sup>33</sup>).

Na dalili ya kwamba kuchinja ni ibada anayostahiki kufanyiwa Allaah tu, ni:

﴿ قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ \* لَا شَرِيكَ لَهُ ﴾

(Sema: Hakika sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Allaah, Mola Mlezi wa viumbe vyote\* hana mshirika<sup>34</sup>).

Na Mtume (Swala na Salamu Zimuendee) amesema:

« وَلَعَنَ اللَّهُ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللَّهِ »

(Allaah amlaani aliechinja kwa kusudia asiye kuwa Allah<sup>35</sup>).

Na dalili ya kwamba isifungwe nadhiri isipokuwa kwa ajili ya Allaah pekee ni:

﴿ يُؤْفُونَ بِالَّذِينَ يَخَافُونَ يَوْمًا كَانَتْ شُرُهُمْ مُسْتَطِيرًا ﴾

(Wanatimiza ahadi, na wanaiogopa siku ambayo shari yake ni yenye kuenea<sup>36</sup>).

---

<sup>32</sup>- Surat An-Naas/1.

<sup>33</sup>- Surat Al-Anfaal/9.

<sup>34</sup>- Surat Al-An'aam/162-163.

<sup>35</sup>- Muslim: (1978).

<sup>36</sup>- Surat Al-Insaan/7.

## **MSINGI WA PILI**

### **MJA KUIJUA DINI YA KIISLAMU KWA DALILI**

**Uislamu ni:** kujisalimisha kwa Allaah kwa kumpwekesha, na kumnyenyenyekea katika kumtii, na kijiepusha na shirki na washirikina, na Uislamu una daraja tatu:

1- Uislamu. 2- Imani. 3- Ihsan.

Na kila daraja moja ina nguzo zake.

### **DARAJA LA KWANZA: NGUZO ZA UISLAMU**

Nguzo za Uislamu ni tano:

- 1- Kukiri kwamba hakuna wa kuabudiwa kwa haki ila Allaah.
- 2- Kisimamisha swala. 3- Kutoa zaka. 4- Kufunga ramadhan. 5- Kuhiji nyumba ya Allaah tukufu (Al-ka'ba).

Dalili ya (kubainisha kwamba) tamko la Laa ilaaha illa Llaahu ni nguzo, ni kauli yake Allaah:

﴿ وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَسِرِينَ ﴾

**(Na anayetafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake.**

**Naye Akhera atakuwa katika wenye hasara<sup>37</sup>).**

Na dalili katika sunna ni hadithi ya Ibn Umar Allaah amridhie:

«بُنِيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ، شَهَادَةِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، وَإِقَامِ الصَّلَاةِ، وَإِيتَاءِ

الزَّكَاةِ، وَحَجِّ الْبَيْتِ، وَصَوْمِ رَمَضَانَ»

---

<sup>37</sup>- Surat Aal Imraan/85.

(Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano, kushuhudia hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki illa Llaahu, na Muhammad ni Mtume wake, Kusimamisha swala, Kutoa zaka, Kuhiji Al-ka'ba, na Kufunga ramadhani<sup>38</sup>).

Na dalili ya kwamba shahada ni nguzo kauli yake Allaah:

﴿شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ  
الْحَكِيمُ﴾

(Allaah, Malaika, na wenye ilimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana, muabudiwa (wa haki) ila Yeye, Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana muabudiwa (wa haki) ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye hikima<sup>39</sup>).

Maana ya neno Laa ilaaha ila Llaahu: hakuna Muabudiwa wa haki ila Allaah.

Na tafsiri yenye kubainisha wazi (maana ya) tamko hili ni kauli ya Allaah:

﴿وَأَدَّ قَالَ إِبْرَاهِيمُ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ إِنَّنِي بَرَاءٌ مِّمَّا تَعْبُدُونَ \* إِلَّا الَّذِي فَطَرَنِي فَإِنَّهُ سَيَهْدِينِ \* وَجَعَلَهَا كَلِمَةً  
بَاقِيَةً فِي عَقْبِهِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ﴾

(Kumbuka pale Ibrahim alipomwambia baba yake na kaumu yake: hakika mimi ninajitenga mbali na hayo mnayo yaabudu\*Isipo kuwa yule aliye niumba, kwani Yeye ataniongoa\*Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika viazi vyake ili warejee<sup>40</sup>).

<sup>38</sup>- Bukhari (8) na Muslim (19).

<sup>39</sup>- Surat Aal-Imraan/18.

<sup>40</sup>- Surat Az-Zukhruf/26-28.

Na kauli ya Allaah mtukufu:

﴿قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ﴾

**(Sema: Enyi Watu wa kitabu! Njooi kwenye neno lilo sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Allaah, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane waabudiwa sisi kwa sisi badala ya Allaah. Na wakikengeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu<sup>41</sup>).**

Na dalili (yenye kuwajibisha) kukiri ya kwamba Muhammad Swala na Salamu Zimuendee ni Mtume wa Allaah ni kauli yake Allaah:

﴿لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ﴾

**(Hakika amekulijieni Mtume anayetokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma<sup>42</sup>).**

Tamko la shahada (Laa ilaaha ila Llaahu) lina nguzo mbili:

**Nguzo ya kwanza:** (لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ) kupinga kila kinachoabudiwa kinyume na Allaah.

**Nguzo ya pili:** (إِلَّا اللَّهُ) inathibitisha ya kwamba Muabudiwa wa haki ni Allaah, wala hana Mshirika katika ibada zake, kama alivyo kuwa hana mshirika katika Ufalme wake.

<sup>41</sup>- Surat Aal-Imraan/64.

<sup>42</sup>- Surat At-Tawba/128.

Na maana ya kukiri ya kwamba muhammad Swala na Salamu Zimuendee ni Mtume wa Allaah ni: kumtii yeye katika yale aliyo amrisha, kumsadikisha kwa yale aliyo sema, kuyaepuka yale aliyo kataza na kuyakemea, na kwamba asiabudiwe Allaah isipokuwa kwa yale aliyoyawekea sheria.

Na dalili ya (kuwa) Swala, Zaka ni nguzo, pamoja na kubainisha tafsiri ya tawhiid ni kauli yake Allaah:

﴿وَمَا أُمْرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ  
وَذَلِكَ دِينُ الْقِيَمَةِ﴾

**(Na hawakuamrisha kitu ila wamuabudu Allaah kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na wasimamishe Swala, na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo Dini madhubuti<sup>43</sup>).**

Na dalili ya kuthibitisha kuwa swaumu ni (nguzo) ni kauli ya Allaah:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ  
لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ﴾

**(Enyi mlio amini mmefaradhishiwa funga kama walivyofaradhishiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kumchamngu<sup>44</sup>).**

Na dalili ya kubainisha kuwa Hija ni (nguzo), ni kauli yake Allaah:

﴿وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ﴾

<sup>43</sup>- Surat Al-Bayyina/5.

<sup>44</sup>- Surat Baqara/183.

(Na “ana Allaah faradhi aliyo iwajibisha” kwa watu “nayo ni” kuhiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakaye kanusha basi Allaah ni mkwasi (simhitaji) kwa walimwengu<sup>45</sup>).

## **NGUZO YA PILI: IMANI**

Imegawanyika mafungu 73 (mpaka 79), ya juu kabisa ni kusema: **(Laa ilaaha illa Llaahu)** na ya chini zaidi ni kuondosha uchafu njiani, na kuona haya (aibu) ni sehemu ya imani.

Na nguzo zake ni sita: Kumuamini Allaah<sup>46</sup>, Malaika<sup>47</sup>, Vitabu<sup>48</sup>,=

---

<sup>45</sup>- Surat Aal Imraan/97.

<sup>46</sup>- Kumuamini Allah kunafungamana na mambo manne:

1. Kuamini kuwepo kwake.
2. Kuamini utendaji kazi wake (Rubuubiyah).
3. Kuamini kwamba Allah pekee ndiye anaestahiki kuabudiwa (Uluuiyyah).
4. Kuamini majina na sifa zake pasina kupotosha maana, kupinga, kumfananisha na viumbe vyake au kuzitafutia namna (kaifiyyah).

<sup>47</sup>- Kuamini Malaika kumefungamana na mambo manne:

1. Kuamini kuwa wapo.
2. Kuamini kwa jumla wale tunao wajua kwa majina yao au wale tusio wajua.
3. Kuamini yale tunayo yajua katika sifa zao.
4. Kuamini yale tunayo yajua katika kazi zao wanazozifanya.

<sup>48</sup>- Kuamini Vitabu kumefungamana na mambo manne:

1. Kuamini kwamba ni kweli vinatoka kwa Allah.
2. Kuamini vile amavyo tumevijua majina yake; kama Qur’an, Injili, Taurat na Zaburi, na pia kuamini vile ambavyo hatuvijui majina yake.
3. Kuzikubali habari zilizotajwa ndani yake, na kuzikubali habari ambazo hazija potoshwa na kubadilishwa katika vitabu vilivyotangulia.
4. Kufanyia kazi hukumu ambazo hazijafutwa, kuridhia na kujisalimisha, ni sawa tumejua hekima yake au hatukujua, na vitabu vyote vilivyo tangulia hukumu zake zimefutwa na Qur’an, kwa hiyo haitofaa kufanyia kazi hukumu yoyote iliyopo ndani yake, ila ile iliyo sahihi na kubaliwa na Qur’an

= Mitume<sup>49</sup>, Siku ya kiama<sup>50</sup>, na Kuamini Qadar heri na shari yake<sup>51</sup>.

Na dalili juu ya nguzo hizi sita ni kauli ya Allaah:

﴿لَيْسَ الْبِرَّ أَنْ تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَكِنَّ الْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ  
وَالْكِتَابِ وَالرَّسُولِ﴾

**(Sio wema kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi. Bali wema ni wa anaye muamimi Allaah na siku ya Mwisho na Malaika na kitabu na Manabii<sup>52</sup>).**

Na dalili ya kuamini Qadar ni kauli ya Allaah:

﴿إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ﴾

**(Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa Qadar<sup>53</sup>).**

---

<sup>49</sup>- Kuamini mitume kumefungamana na mambo manne:

1. Kuamini kuwa wametumwa na Allaah, kwa hiyo kukanusha utume wa mmoja wao ni sawa na kuwakanusha wote.
2. Kuamini wale tulio wajua majina yao, mfano Muhammad, Ibrahim swala na Salamu Ziwaendee n.k. na pia wale tusio wajua majina yao.
3. Kukubali yale yaliyosihia kutoka kwao katika habari zao.
4. Kufanyia kazi sheria za Mtume Swala na Salamu Zimuendee aliye tumwa kwetu.

<sup>50</sup>- Siku ambayo watu watafufuliwa kwa ajili ya hisabu na malipo, na imeitwa siku ya mwisho kwa sababu hakuna tena siku baada yake, kiasi ambacho watu wa peponi watabaki humo milele, na watu wa motoni kadhalika.

<sup>51</sup>- Kuamini Qadar kunafungamana na mambo manne:

1. Kuamini kwamba Allaah ameshajuwa kila kitu kwa jumla na ufafanuzi, ni sawa kwa yanayo fungamana na vitendo vyake au vya waja wake.
2. Kuamini kwamba hayo yote Allaah ameyaandika kwenye Lauhil Mahfudh.
3. Kuamini kwamba hakuna kinachotokea isipokuwa kwa matashi yake.
4. Kuamini kwamba kila kinachotokea Allaah ndiye aliye kiumba.

<sup>52</sup>- Surat Al-Baqara/177.

<sup>53</sup>- Surat Al-Qamar/49.

## NGUZO YA TATU NI: IHSAAAN

Nayo ina nguzo moja tu, ambayo ni kumuabudu Allaah kama unamuona, na ikiwa humuoni basi (tambua) kuwa yeye anakuona.

Na dalili ni kauli ya Allaah:

﴿إِنَّ اللَّهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوْا وَالَّذِينَ هُمْ مُحْسِنُونَ﴾

(Hakika Allaah yu pamoja na wenye kumcha, na watendao mema<sup>54</sup>).

Na kauli yake Allaah:

﴿وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ \* الَّذِي يَرِيكَ حِينَ تَقُومُ \* وَتَقَلُّبِكَ فِي السَّجِدِينَ \* إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ﴾

(Na mtegemee (Allaah) Mwenye nguvu Mwenye kurehemu\* Ambaye anakuona unapo simama\*Na mageuko yako kati ya wanao sujudu\*hakika

Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua<sup>55</sup>).

Na kauli yake Allaah:

﴿وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ﴾

(Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika qur'ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo<sup>56</sup>).

<sup>54</sup>- Surat An-Nahli/128.

<sup>55</sup>- Surat As-Shua'raa/217-220.

<sup>56</sup>- Surat Yunus/61.

Na dalili katika sunna ni hadithi ya Jibril iliyo mashuhuri: Kutoka kwa Umar Bin Khattwab Allaah amridhie amesema: [Siku moja tukiwa tumekaa mbele ya Mtume Swala na Salamu Zimfikie punde alitokea mtu mmoja, nguo zake ni nyeupe sana, nywele zake nyeusi sana, wala haionekani juu yake alama ya safari, na wala hakuna miongoni mwetu anayemjua, mpaka akakaa mbele ya Mtume Swala na Salamu Zimfikie, akaegemeza magoti yake kwenye magoti ya Mtume Swala na Salamu Zimfikie, akasema: Ewe Muhammad, nifahamishe kuhusu uislamu, akasema Mtume: **“uislamu ni kukiri kwamba hakuna wa kuabudiwa kwa haki ila Allaah, na kwamba Muhammad ni Mtume wake, kusimamisha swala, kutoa zaka na kuhiji nyumba (Al- kaaba) ukiweza kuindea njia hiyo”**]. Akasema Jibril: umesema kweli. Amesema (Umar Allaah amridhie): tukamshangaa, anamuuliza halafu anamsadikisha. Akasema (Jibril): Nifahamishe kuhusu Imani, akasema (Mtume Swala na Salamu Zimfikie): **[Imani ni kumuamini Allaah, malaika wake, vitabu vyake, Mitume wake, siku ya mwisho, na kuamini qadar<sup>57</sup> kheri yake na shari yake]**. Akasema (Jibril): umesema kweli. Akasema: Nifahamishe kuhusu ihsaan, akasema (Mtume Swala na Salamu Zimfikie) ni **[kumuabudu Allaah kama unamuona, na ikiwa humuoni basi yeye anakuona]**. Akasema (Jibril): nifahamishe kuhusu kiama. Akasema (Mtume Swala na Salamu Zimfikie): **[hakuwa anaye ulizwa ni Mjuzi zaidi wa hicho (kiama) kuliko anaye uliza]**. Akasema (Jibril): Nifahamishe dalili zake. Akasema: **[mtumwa kumzaa bwana wake<sup>58</sup>, na utawaona watu wakienda (peku) bila viatu, wakienda uchi, Masikini na Wachunga mbuzi wakirefusha**

---

<sup>57</sup>- Makadario ya Allaah kwa viumbe yametangulia kwa miaka Eflu 50 kabla hajawaumba.

<sup>58</sup>- Kuna maana mbili kuhusu maneno haya:

1. Mjakazi atafanya jimai na Sayyid wake kisha atazaliwa naye na huyo mtoto naye pia ni bwana, kwa sababu hukumu yake ni kama baba yake.
2. Ishara ya kuharibika kwa maadili kiasi mtoto atamkaripia mzazi wake, na mzazi hatoweza kumkemea mwanae kwa kumuogopa, hapo mtoto ni sawa na Sayyid.

**majengo**<sup>59</sup>. Amesema (Umar Allaah amridhie): akaondoka, nikabaki nimeshangaa, kisha (Mtume Swala na Salamu Zimfikie) akaniambia: **[Ewe Umar: Je unamjua yule muulizaji?]**. Nikasema: Allaah na Mtume wake wanajua zaidi, akasema: **[hakika yule ni jiblr amekujieni ili awafundishe dini yenu**<sup>60</sup>].

## **MSINGI WA TATU KUMJUA MTUME WENU MUHAMMAD (Swala na Salamu Zimuendee)**

Naye ni Muhammad Ibn Abdillaahi Bin Abdil Muttwalib Bin Hashim, na Hashim anatokana na Kureish, na Kureish anatokana na waarabu ambao ni kizazi cha Ismail Bin Ibrahim Al-khalil Swala na Salamu Ziwaendee.

Amefariki akiwa na miaka (63), miaka (40) kabla ya Utume na miaka (23) akiwa ni Nabii na Mtume. Na amepewa Unabii kwa kuteremshiwa surat Al-Muddaththir na Utume kwa kuteremshiwa surat Al-Muzzammil. Na mji wake aliozaliwa ni Makka, kisha alihama kwenda Madina.

Allaah alimtuma kwenda kukemea shirki, na kulingania kwenye tawhiid, na dalili ni kauli yake:

﴿ يَا أَيُّهَا الْمَدِينُ \*\* قُرْ فَأَنْذِرْ \*\* وَرَبِّكَ فَكَبِّرْ \*\* وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ \*\* وَالرُّجْزَ فَاهْجُرْ \*\* وَلَا تَمْنُنْ  
تَسْتَكْبِرُ \*\* وَلِرَبِّكَ فَاصْبِرْ ﴾

---

<sup>59</sup>- Watu wa kawaida (kipato cha chini) watakuwa wanashindana kujenga majengo ya kifahari.

<sup>60</sup>- Muslim namba: (8).

**(Ewe uliyejigubika\*Simama uonye\*Na Mola wako Mlezi mtukuze! \*Na nguo zako zisafishe\*Na yaliyo machafu yahame\*Wala usitoe kwa kutaraji kuzidishiwa\*Na kwa ajili ya Mola wako Mlezi, subiri!<sup>61</sup>).**

**Ufafanuzi wa aya katika surat Al-Muddatthir:**

Maana ya kauli yake:

﴿فُرُفَانَذِرْ﴾

**(Simama uonye)**

Aonye kutokana na shirki na alinganie kwenye Tauhid.

﴿وَرَبِّكَ فَكَبِّرْ﴾

**(Na Mola wako Mlezi mtukuze).**

Mtukuze kwa tauhid na mpwekeshe.

﴿وَوِيَابِكَ فَطَهِّرْ﴾

**(Na nguo zako zisafishe).**

Zitakase amali zako kutokana na shirki.

﴿وَالرُّجُزَ فَاهْمِجْ﴾

**(Na yaliyo machafu yahame).**

Na maana ya neno: **الرُّجُزُ** (Ar Rujzu) ni: (Masanamu), na kuyahama kwake ni kuyaacha na kujiepusha nayo, pamoja na

---

<sup>61</sup>- Surat Al-Muddatthir/1-7.

kujitenga na wenye watu wa Masanamu.

Alifanya kazi hiyo kwa muda wa miaka kumi, analingania kwenye tawhiid, na baada ya miaka kumi alipandishwa mbinguni na kufaradhishiwa swala tano.

Aliswali akiwa Makka miaka mitatu, na baada ya hapo aliamrisha kufanya Hijra (kuhama) kwenda Madina.

**Ufafanuzi katika kubainisha maana ya Hijra na kuwa kwake ni yenye kuendelea:**

**Hijra ni:** kuhama mji wa shirki (kufuru) kwenda mji wa kiislamu. Na Hijra itaendelea mpaka siku ya kiyama kwa kauli ya Allaah:

﴿ إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّاهُمُ الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنْفُسِهِمْ قَالُوا فِيمَ كُنْتُمْ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّهِ وَسِعَةً فَتُهَاجِرُوا فِيهَا فَأُولَئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ وَسَاءَتْ مَصِيرًا \* إِلَّا الْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ لَا يَسْتَطِيعُونَ حِيلَةً وَلَا يَهْتَدُونَ سَبِيلًا \* فَأُولَئِكَ عَسَى اللَّهُ أَنْ يَعْفُوَ عَنْهُمْ وَكَانَ اللَّهُ عَفُورًا ﴾

**(Hakika Malaika watawaambia wale ambao wamewafisha hali ya kuwa wamezidhulumu nafsi zao: Mlikuwa vipi? Watasema: Tulikuwa tunaonewa. Watawaambia: kwani ardhi ya Allaah haikuwa na wasaa mkahamia humo? Basi hao makazi yao ni Jahannamu, nayo ni marejeo mabaya kabisa\*Isipokuwa wale walio kuwa wanyonge miongoni mwa wanaume na wanawake na watoto wasio na uwezo wa hila ya kuongoza njia yakuhama\*Basi hao huenda Allah atawasamehe. Na Allaah ni mwingi wa kusamehe, Mwingi wa maghfira<sup>62</sup>).**

<sup>62</sup>- Surat An-Nisaa/97-99.

Na kauli yake Allaah:

﴿يَعْبَادِي الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ أَرْضِي وَاسِعَةٌ فَإِنِّي فَاعْبُدُونِ﴾

**(Enyi waja wangu mlio amini! kwa hakika ardhi yangu ina wasaa. Basi niabuduni Mimi peke yangu<sup>63</sup>).**

Na dalili katika sunna ya (kuelezea ulazima wa) Hijra ni kauli ya Mtume Swala na Salamu Zimfikie:

**(Hijra haitokoma mpaka ikatike toba, na toba haikatiki mpaka litapochomoza jua upande wa magharibi<sup>64</sup>).**

**Ufafanuzi katika kubainisha matunda yaliyopatikana baada ya kuhami Madina:**

Wakati alipokuwa ametulizana katika mji wa Madina, alipewa sheria ya amri nyingine zilizobaki, mfano: Zaka, Funga, Hija, Jihad, Adhana, kuamrisha mema na kukataza maovu, (na nyingine katika sheria za kiislamu).

Alifanya hivyo kwa muda wa miaka kumi (kisha) alifariki Mtume Swala na Salamu Zimfikie, lakini dini yake ni yenye kubaki, na hii ndio dini yake, hakuna kheri yoyote isipokuwa ameufahamisha umma (wake), na hakuna shari isipokuwa ameuhadharisha

---

<sup>63</sup>- Surat Al-Ankabuut/56.

- Amesema Ibn Kathir Allaah amrehemu kuhusu aya hii: "Hii ni amri kutoka kwa Allaah kwa waja wake waislamu, kwamba wahame kutoka mji ambao hawana uwezo ndani yake wa kusimamisha dini, wahamie ardhi ya Allaah yenye wasaa, ambayo wanaweza (ndani yake) kusimamisha dini, ili wampwekeshe Allaah na wamuabudu kama alivyo waamrisha, ndio maana akasema:

﴿يَعْبَادِي الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ أَرْضِي وَاسِعَةٌ فَإِنِّي فَاعْبُدُونِ﴾

**(Enyi waja wangu mlio amini! kwa hakika ardhi yangu ina wasaa. Basi niabuduni Mimi tu).**

<sup>64</sup>- Sunan Abi Daud: (2479).

nayo, na kheri kubwa ambayo ameufahamisha umma ni tawhiid na yote ambayo Allaah anayapenda na kuyaridhia, na shari kubwa ambayo ameuhadharisha nayo umma ni shirki na yote ambayo Allaah anayachukia na kuyakataa.

Allaah alimtuma kwenda kwa watu wote, na pia akafaradhisha kwa majini na watu kumtii yeye.

Na dalili ni kauli ya Allaah:

﴿قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا﴾

**(Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote<sup>65</sup>)-**

Na Allaah amekamilisha kupitia kwake dini, na dalili ni kauli yake:

﴿الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتَمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا﴾

**(Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimeridhia kwenu Uislamu uwe ndo dini<sup>66</sup>)-**

Na dalili yeye kufahamisha ya kuwa Mtume Swala na Salamu Zimfikie atakufa ni kauli ya Allaah:

﴿إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُمْ مَيِّتُونَ \* ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عِنْدَ رَبِّكُمْ تَخْتَصِمُونَ﴾

**(Kwa hakika wewe utakufa, na wao watakufa\*\*kisha bila ya shaka Siku ya kياما mbele ya Mola wenu Mlezi mtahasimiana<sup>67</sup>)-**

---

<sup>65</sup>- Surat Al-A'raaf/158.

<sup>66</sup>- Surat Al-Maida/3

<sup>67</sup>- Surat Az-Zumar/30-31.

**Ufafanuzi wa kubainisha mambo yanayo patikana baada ya kufa:**

Na watu baada ya kufa watafufuliwa.

Na dalili ni kauli yake Allaah:

﴿ مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ ﴾

**(Kutokana na (ardhi) tumekuumbeni, na humo tunakurudusheni, na kutoka humo tutakutoeni mara nyingine<sup>68</sup>).**

Na kauli yake:

﴿ وَاللَّهُ أَنْبَتَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ نَبَاتًا \* ثُمَّ يُعِيدُكُمْ فِيهَا وَيُخْرِجُكُمْ إِخْرَاجًا ﴾

**(Na Allaah amekuotesheni katika ardhi mimea\*\*Kisha atakurudisheni humo na atakutoeni tena<sup>69</sup>).**

Na baada ya kufufuliwa watahesabiwa na kulipwa kwa amali zao.

Na dalili ni kauli yake Allaah:

﴿ وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَوُوا بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَىٰ ﴾

**(Ni vya Allaah vyote viliomo mbinguni na ardhini, ili awalipe walio tenda ubaya kwa waliyo yatenda, na walio tenda mema awalipe mema<sup>70</sup>).**

---

<sup>68</sup>- Surat Twaha/55.

<sup>69</sup>- Surat Nuhu/17-18.

<sup>70</sup>- Surat An-Najm/31.

**Ufafanuzi katika kuelezea hukumu ya kupinga mambo yanayokuja baada ya kufa:**

Na mwenye kupinga kufufuliwa amekufuru.

Na dalili ni kauli ya Allaah:

﴿ زَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ لَنْ يُبْعَثُوا قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ وَذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴾

**(Wamedai walio kufuru kuwa hawatafufuliwa. Sema: Kwanini?**

**Naapa ka wangu Mlezi hapana shaka mtafufuliwa, na kisha mtaambiwa mliyo yatenda. Na hayo ni mepesi kwa Allaah<sup>71</sup>).**

**Ufafanuzi katika kubainisha hekima ya kupelekwa Mitume:**

Na Allaah amewatuma manabii wote kwenda kutoa bishara na kuonya, na dalili ni kauli yake Allaah:

﴿ رُسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ﴾

**(Hao ni Mitume wabashari na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Allaah baada ya kuletewa Mtume<sup>72</sup>).**

Na Mtume wa kwanza ni Nuhu Swala na Salamu Zimuendee, na wa mwisho wao ni Muhammad Swala na Salamu Zimuendee.

Na dalili ya kwamba Nabii wa kwanza ni Nuhu ni kauli yake Allaah:

﴿ إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَىٰ نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ ﴾

**(Hakika Sisi tumekuletea wahyi wewe kama tulivyo wapelekea wahyi Nuhu na Manabii walio kuwa baada yake<sup>73</sup>).**

---

<sup>71</sup>- Surat Ttaghaabun/7.

<sup>72</sup>- Surat An-Nisaa/165.

<sup>73</sup>- Surat An-Nisaa/173.

**Ufafanuzi katika kubainisha kwamba Allaah alipeleka kwa kila umma Mtume (ili kusimamisha hoja juu yao):**

Na kila umma Allaah aliwapelekea Mtume, tangu zama za Nuuh Swala na Salamu Zimuendee mpaka zama za Mtume Muhammad Swala na Salamu Zimuendee, (akawa) anawaamrisha watu wamuabudu Allaah pekee, na anawaonya wamuepuke shetani.

Na dalili ni kauli yake Allaah:

﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الزَّلَّاتِ﴾

**(Na kwa hakika kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Allaah,na muepukeni Shetani<sup>74</sup>).**

**Ufafanuzi katika kubainisha kile alichofaradhisha Allaah kwa waja wake:**

Allaah amefaradharisha kwa waja wake wote kumkanusha shetani, na kumuamini Allaah peke yake.

Amesema Ibnul Qayyim (Allaah amrehemu): **(Twaghuut ni kila ambaye mja amevuka mipaka kwa ajili yake kwa kumuabudu, au kwa kumfuata na kumtii (katika mambo ya harammu<sup>75</sup>))**

Na Twaghuut ni wengi, lakini viongozi wao ni watano:

- 1- Iblis Allaah amlaani.
- 2- Mwenye kuabudiwa naye akaridhia.
- 3- Mwenye kuwaita watu kwenye kumuabudu yeye.
- 4- Mwenye kudai (kuwa anajua) kitu katika elimu ya ghaibu.
- 5- Mwenye kuhukumu kinyume na alivyoteremsha Allaah.

<sup>74</sup>- Surat An-Nahli/36.

<sup>75</sup>- l'laamul Muwaqqi'n (Jz. 1, Uk. 74).

Na dalili ni kauli ya Allaah:

﴿لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ قَدْ تَبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ فَمَنْ يَكْفُرْ بِالطَّاغُوتِ وَيُؤْمِنْ بِاللَّهِ فَقَدِ اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقَى﴾

[Hapana kulazimisha katika Dini, kwani Uongofu umekwisha pambanuka na Upotofu. Basi anaye mkataa shetani na akamuamini Allaah hakika amekamata kishikio madhubuti<sup>76</sup>].

Na hii ndiyo maana ya Laa ilaha illaLlaahu (Hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki ila Allaah).

Na imekuja katika hadithi:

(رَأْسُ الْأَمْرِ الْإِسْلَامُ، وَعَمُودُهُ الصَّلَاةُ، وَذِرْوَةٌ سَنَامِهِ الْجِهَادُ)

[Kichwa cha Dini ni Uislamu (kutamka Laa ilaaha ilaLlaahu), na nguzo yake ni swala, na kilele cha nundu yake ni Jihad<sup>77</sup>].

Na Swala na Salamu Zimuendee Mtume Muhammad.

Wabilaahi Ttaufiq.

**Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud**  
**(Allaah amsamehe yeye na wazazi wake)**  
**5/Jumaadal Aakhira/1439<sup>H</sup> – 21/2/2018<sup>M</sup>**  
**Pongwe Tanga**  
**Tanzania.**

**Simu: 0715263253.**  
**Shayhat033@gmail.com**

<sup>76</sup>- Surat Al-Baqara/256.

<sup>77</sup>- Sunan Tirmidh (Jz. 4, Uk. 308).